Ninayo furaha kukueleza kuwa, tangu kuanzishwa kwa NeST, Julai 1, 2023, matokeo makubwa ya kiuchumi na kijamii yamepatikana, kwani mikataba yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Trilioni 14.9 imetolewa kwa wazabuni kupitia mfumo huo. Mabadiliko haya pia yamegusa maisha ya watanzania wote, kwa kutoa fursa za zabuni za upendeleo kwa ajili ya makundi maalum (wanawake, wazee, vijana na watu wenye mahitaji maalum). Hadi toleo hili linachapishwa, mikataba ya zabuni yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 11 imekwishatolewa kwa makundi maalum, kupitia NeST, hivyo kuongeza fursa za kutoa ajira kwa watanzania wengi zaidi.

Toleo hili linachapisha taarifa za matukio kadhaa muhimu katika sekta ya ununuzi wa umma, pia lina makala itakayokuelimisha na kukuongeza uelewa kuhusu jinsi ya kutumia fursa zinazopatikana kutokana na mapinduzi ya teknolojia na mabadiliko ya sheria ya ununuzi wa umma.

Aidha, napenda kukufahamisha kuwa Serikali imeendelea na jitihada zake katika kuwasogezea huduma wananchi, ambapo kupitia PPRA tumefungua ofisi katika kanda sita nchini: Mwanza kwa ajili ya Kanda ya Ziwa, Arusha kwa ajili ya Kanda ya Kaskazini, Mtwara kwa ajili ya Kanda ya Kusini, Mbeya kwa ajili ya Nyanda za Juu Kusini, na Tabora kwa ajili ya Kanda ya Kati.

Serikali inavyozidi kujikita katika matumizi ya teknolojia, imeweza kuibuka na matumizi mahsusi ya kidijitali kwenye ununuzi wa umma na kweli yameongeza ufanisi na uwazi katika maeneo yote. Nakualika ujisomee mengi yaliyomo humu ili uweze kujiandaa kufaidi mabadiriko chanya yaliyomo katika ununuzi wa umma nchini.

Ni dhahiri kuwa kuna nafasi kwa kila mdau wa ununuzi wa umma kufaidika kwa namna moja au nyingine katika fursa zinazopatikana na kuwawezesha wadau wote nchini kuungana katika kushangilia mapinduzi yaliyoletwa na Serikali ya Awamu ya Sita.

KUTOKA KWA MHARIRI

Ni waadilifu pekee watakaona tija ya NeST wengine wataona adha tu

“Sheria bora ni ile iliyomo nafsini mwako, na hivyo hivyo kwa mfumo bora. Kama nafsini mwako hakuna mfumo, utakaoundiwa na ulimwengu utautumia vibaya.” – Rais Samia Suluhu Hassan

Awali ya yote, kabla ya kuzama kwenye mada ya safu hii – ikiwa ni mahsusi kwa toleo la kwanza la TPJ babukubwa - tunayo heshima kutambua michango ya watu wawili, iliyonogesha tafakuri: Rais Samia Suluhu Hassan, aliyetamka maneno yaliyopo hapo juu, na Waziri wa Fedha Mwigulu Nchemba, aliyechangia katika kuyasambaza kwa upana na urefu, alipomnukuu wakati akipokea ripoti ya mwaka ya PPRA kwa mwaka 2023/24.

Nukuu hii maridhawa, ina mvuto wa kipekee kwa sababu iko katika staili inayofunua uadilifu kimafundisho na kutujavya jinsi ya kutenda sawa na haki katika mambo yote – ikiwa ni pamoja na ununuzi wa umma.

Hivyo basi, litakuwa jambo jema kama somo lake litasambaa na kuwa endelevu, bila kuchuja wala kuisha makali, katika vyombo vya habari na katika makongamano – hasa ya ununuzi wa umma - kwa sababu ‘upigaji’ na uadilifu havipikiki chungu kimoja vikaiva.

Kila mpenda uadilifu anayo namna ya kuchangia katika kusambaza somo hili; kama alivyofanya Waziri Mwigulu, alipotufungua macho kuhusu alichokisema Rais Samia kwa kumnukuu, katika kukoleza karipio dhidi ya watendaji walioanza tabia ya kuchonga sababu za kuelezea kwa nini hawatumii NeST, wakati sababu halisi ni kufanikisha ubadhirifu kwa manufaa yao binafsi.

Kuibuka kwa tabia za namna hii, zinazokwamisha mipango ya Serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo, kunahitaji mjadala mpana. Mfano: kama si kwa nia ovyo ya kujipatia pesa, yawezekana vipi afisa apinge matumizi ya NeST – mfumo uliojengwa mahsusi ili kumrahisishia kazi na kuleta tija katika shughuli aliyoajiriwa kuifanya? Aidha, katika muktadha huu, anawezaje kutaka kukwamisha mipango ya Serikali, inayolenga kuboresha maisha ya wananchi wengi – akiwamo yeye mwenyewe, ndugu na majirani zake?

Haya yote ni maswalamsingi ya kimaadili yanayogusa uadilifu, hivyo yanastahili kupewa kipaumbele katika mjadala na makongamano ya wadau wa ununuzi wa umma, fursa inapojitokeza.

Kwa bahati nzuri, fursa ya namna hii aliipata tena Mwigulu, alipokwenda kufunga kongamano la kumi na sita la jukwaa la ununuzi wa umma Afrika Mashariki, jijini Arusha ambapo, aliwaasa wadau kuchangamkia “utumiaji wa mifumo” na kutii sheria ya ununuzi.

Lakini, yawezekana kuna walengwa ambao hawakumpata vizuri Mwigulu; kwa ajili yao tunatanabahisha hapa kwamba, kauli yake imejikita katika kuhimiza uadilifu kwa wanaununuzi wa umma, hata akamnukuu Rais Samia katika kusisitiza jambo hilo. Na ukichukulia kwamba kongamano husika lilikuwa limejadili utumiaji wa mifumo katika ununuzi wa umma, kauli ile inaendana vizuri na karipio lake la awali dhidi ya wapinga NeST.

KUTOKA KWA MHARIRI...

Aghalabu, huwa rahisi kwa mtu kuelekeza lawama kwa watu wengine, hivyo si ajabu kusikia watendaji wabadhirifu wakitamani ikubalike kuwa ‘matatizo ya kiteknolojia’ ndiyo sababu pekee ya wao kutokutumia NeST – wala si ulafi wao wa pesa, uliopitiliza kiasi cha kuwafanya wapoteze tunu ya uadilifu waliyopewa na Muumba.

Cha kufanya? Tubadilike. Ni kweli sote tunapenda mabadiriko chanya katika maisha yetu – ndivyo tulivyoumbwa ila shida ni kwamba baadhi yetu wanapenda mabadiriko hayo yaje bila wao kubadirika katika nafsi zao! Kuna mvutano hapa: Tunapenda mfumo utuletee tija na mishahara minono – lakini bila sisi kubadirika kitabia. Kwa maneno mengine, tunataka tufurahie tija ya NeST huku tukiwa tumenuna kwa vile imetuharibia ulaji!

Ukiirejea ile nukuu, utagundua haya:

Sheria bora ni iliyotoka kwa Mungu; mfumo bora ni ule asilia yaani maadili (au uadilifu); NeST ni mfumo ulioundwa na binadamu, kama huna uadilifu, utauhujumu.

Hitimisho:

Hakika kuogopa jambo jipya kwa sababu ya kutolijua, ni hulka ya binadamu. Lakini kuogopa NeST kimbini ili ujitajirishe binafsi, ni jambo linalotishia mustakabali wa taifa. Hivyo, kama tunataka maisha mazuri kwa ajili yetu na kwa ajili ya wengine, tuanze na ujasiri wa kurejesha mfumoasilia katika nafsi zetu.

Rais Samia afurahishwa na mgawo wa 30% ya tenda kwa makundi maalum



Rais Samia Suluhu Hassan amesema kuwa amefurahishwa na mwitikio wa taasisi za Serikali kwa kutenga na kutoa asilimia 30 ya bajeti za ununuzi kwa ajili ya makundi maalum katika jamii.

Rais Samia ameyasema hayo katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, yaliyofanyika kitaifa katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, 8 Machi 2025, jijini Arusha.

Amesema jambo hilo limewezekana kupitia sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 iliyoweka sharti kwa taasisi nunuzi kutenga asilimia 30 ya zabuni zote kwa ajili ya makundi maalum ikiwa ni pamoja na wanawake.

“Nimefurahishwa sana... juzi nikiwa napokea taarifa ya Sekta ya Ujenzi na Miundombinu wakaniambia kwamba kuna kazi kadhaa za barabara zimetolewa, na asilimia 30 ya kazi hizo wamepewa wakandarasi wanawake,” alisema Rais Samia na kuelekeza kuwa hatua kama hii ifanyiike kwenye maeneo mengine pia.

Inafahamika kwa wadau pia kwamba Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 inaelekeza kuwa fursa za zabuni, ikiwa ni pamoja na asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi wa umma katika taasisi za Serikali, itengwe kwa ajili ya makundi maalum na zitolewe kupitia NeST.

Watanzania wanaweza kuunda vikundi vya watu 5 mpaka 20, vikasajiliwa kwenye halmashauri zao na baadaye kwenye NeST ili kuomba zabuni zilizotengwa kwa ajili yao.

Hivi karibuni, Mkurugenzi Mkuu wa PPRA, Bw. Dennis Simba alisema kuwa NeST, iliyoanza kutumika Julai 1, 2023 ni matunda ya jitihada mahsusi za Rais Samia aliyefanikisha kupatikana kwa Sheria ya Ununuzi ya Mwaka 2023 na kutanabahisha kwamba hadi kufikia Februari 2025 makundi maalum yalipata zabuni zenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 11.

Pia, alieleza kuwa makundi 66 ya wanawake yalipata zabuni 146 zenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 5.6, na kwamba kiasi kilichobaki kimeenda kwa makundi mengine.

Makamu wa Rais aagiza NeST itumike kudhibiti ubadhirifu

Makamu wa Rais Dkt. Phillip Mpango ameagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kuhakikisha ununuzi wa umma unafanyika kupitia mfumo wa kielektroniki – NeST, ili kudhibiti vitendo vinavyosababisha ubadhirifu na upotevu wa fedha za umma.

Dkt. Mpango alitoa maelekezo hayo Februari 11, 2025, alipotembelea banda la PPRA kabla ya kufungua Mkutano wa Tano wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), unaofanyika jijini Arusha katika ukumbi wa mikutano AICC, Februari 11 – 13, 2025.

Akizungumza baada ya Mkurugenzi Mkuu wa PPRA, Bw. Dennis Simba, kuelezea ufanisi wa NeST ulioanza kutumika Julai 1, 2023, Makamu wa Rais alisema anaamini matumizi ya mfumo thabiti ya kielektroniki yanaweza kudhibiti ubadhirifu unaofanywa na baadhi ya watu aliowafananisha na mchwa.



“Nikiangalia ripoti [za ukaguzi] za PPRA, sipendezwi... na mimi naamini kwamba mfumo thabiti ya kimtandao itatusaidia kudhibiti wale mchwa wanaotuharibia ununuzi. Unajua... katika bajeti ya taifa, karibu asilimia 80 ni kwa ajili ya ununuzi. Kwa hiyo, nategemea PPRA mtusaidie kupunguza au kuondokana kabisa na hayo matatizo,” alisema Dkt. Mpango.

“Ninyi wataalam wa IT [TEHAMA] PPRA, chukueni ripoti moja, kwa mfano ya mwaka jana, halafu ainisheni yale matatizo makubwa ni ya aina gani, na jinsi mfumo itakavyotusaidia kupambana nayo.”

Aidha, Makamu wa Rais aliipongeza PPRA kwa jitihada zake katika kudhibiti ununuzi wa umma nchini.

Naye Bw. Simba alieleza kuwa PPRA imeanza kutekeleza maelekezo hayo kwa kuweka vizuizi vya ki-Tehama kwenye NeST ili kukabiliana na udanganyifu na ubadhirifu uliowekwa bayana kwenye ripoti za ukaguzi, ili mfumo huo, ambao tangu ulipoanziswa umekwishatoa mikataba yenye thamani ya takribani Shilingi trilioni 14, uongeze upatikanaji wa thamani ya fedha.

Makamu wa Rais aagiza NeST itumike kudhibiti...

Ndani ya NeST tumeweka magezi yanayozuia wahalifu wasiweze kupita na hata wakipita watambulike,” alisema Bw. Simba na kutoa mifano kwamba sasa mkataba hauwezi kamwe kutoka bila kusainiwa na bodi ya zabuni, na pia kwamba ni lazima ripoti ya kamati ya tathmini isainiwe na wajumbe husika.

Aidha, Bw. Simba alitaja changamoto inayojitokeza hivi sasa kuwa ni kukosekana kwa uelewa na elimu kwa umma ambapo Mamlaka hiyo inaendelea na jitihada za kutoa elimu kwa wadau, ikiwa ni pamoja na kutumia mtandao ili kuongeza kasi ya kuwafikia walengwa wote.

Makamu wa Rais pia alikabidhi PPRA tuzo ya kutambua nafasi ya PPRA kama mmoja wa wadhamini wakuu wa Mkutano wa Tano wa Mamlaka ya Serikali Mtandao.

Mwigulu: Tanzania iko tayari kusaidia Afrika ifikie ununuzi wa umma kidijitali

Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, amesema Tanzania iko tayari kushirikiana na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi nyingine barani, ili kuhakikisha zinapiga hatua pamoja kufanikisha ununuzi wa umma kupitia mifumo ya kidijitali, TPJ imebaini.

Dkt. Nchemba, aliweka wazi utayari huo katika hotuba aliyotoa, akimwakilisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, katika kufunga Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki, jijini Arusha.

Katika hotuba hiyo, Dkt. Nchemba alisema kuwa wakati nchi inasonga mbele katika kuwaletea maendeleo wananchi huku ikiwa tayari imekijikita katika matumizi ya mifumo ya kidijitali, itahakikisha inaenda sambamba na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

“Tunatamani tuwe pamoja kwenye mifumo hii ya kidijitali, na kwa vile Tanzania iko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na SADC, ni kiungo kinachoweza kuleta tija katika jitihada za kuunganisha mifumo ya nchi zote hizi,” alisema Dkt. Nchemba na kusisitiza: “Tuko tayari kuwezesha jambo hili kwani tunatamani twende Pamoja katika mifumo hii.”

Aidha, ametoa wito kwa serikali zote barani Afrika kuhakikisha sheria zao za ununuzi zinalinda na kutoa upendeleo kwa ajili ya matumizi ya bidhaa, kampuni, na watu walioko barani kabla ya kuwafaidisha walioko nje.

Mwigulu: Tanzania iko tayari kusaidia Afrika ifikie...



“Kutokana na mkutano huu, tuchangamkie uzalendo. Sheria yetu ya ununuzi ielekeze kwamba tuwe tunatumia bidhaa zinazozalishwa barani Afrika kwanza mpaka pale tu zinapokuwa hazipatikani Afrika. Kila mahali tujivunie bidhaa na ubunifu wetu - hata kwenye ujenzi - tutumie bidhaa zinazopatikana hapa Afrika tu; za nje ya bara letu tuzitumie pale tu tusipokuwa na mbadala kutoka ndani,” alisema.

Katika hatua nyingine, Dkt. Nchemba amesema kuwa pamoja na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 kuzitaka taasisi zote za umma zitumie mfumo wa kielektroniki, NeST, lengo likiwa kuutumia kuongeza ufanisi na upatikanaji wa thamani halisi ya fedha, siyo kamwe kuwa mbinu ya kukwamisha maendeleo ya wananchi. Katika kusesitiza jambo hilo,

Aidha, aliwaaasa washiriki wa kongamano kutafakari kwa kina busara inayobebwa na nukuu mahsusi ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhusu namna bora ya kuzingatia sheria na mifumo kiuzalendo, akisema: “Sheria iliyo bora zaidi ni ile iliyoandikwa nafsini mwako, na mfumo ulio bora ni ule ulioandikwa nafsini mwako. Mfumo usipokuwa nafsini mwako, utauchezesha sana mfumo huo uliondaliwa kwa ajili yako.”

“Upatikanaji wa thamani halisi ya fedha kwenye miradi inayotekelezwa ndio unaozaa uaminifu wa wananchi kwa Rais wao, na ndio maana nchi inaendelea kutekeleza miradi mikubwa kwa ufanisi,” alisema Dkt. Nchemba.

Kongamano hilo, lililoratibiwa na PPRA na kubeba kaulimbiu “Matumizi ya Dijitali kwa Ununuzi wa Umma Endelevu,” lilifanyika jijini Arusha na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 1,000 kutoka nchi nane za Afrika Mashariki na nchi nyingine.

Manasseh apangua maswali ya Clouds FM kuhusu PPRA, NeST

Meneja wa PPRA Kanda ya Mtwara, Finias Manasseh, amefafanua kimahiri maswala kadhaa kuhusu PPRA, ununuzi wa umma na NeST katika mahojiano ya kushtukiza na kituo cha redio Clouds FM, mubashara kutoka kwenye banda la maonyesho la PPRA katika manispaa ya Mtwara-Mikindani, Oktoba 23, 2024, TPJ imebaini.

Akiwa anahudumu kwenye banda wakati wa kampeni ya Malkia wa Nguvu – Mtwara, Manasseh alikuwa akijibu hoja za wageni mbalimbali, akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Abdallah Mwaipaya, alipojikuta akihojiwa mubashara na Clouds FM, juu ya maswala kadhaa kuhusu PPRA na ununuzi wa umma.



Baadaye kidogo ikawa wazi kwamba Manasseh, ambaye ni mzoefu wa kujibu maswali juu ya mambo haya, alikuwa akijisikia raha pale alipokuwa akiulizwa maswali yaliyokuwa yamekaa kimtego kutoka kwa Mwaipaya, ambaye kumbe ni mtangazaji mzoefu, anayejua kuibua majibu yenye kuelewesha na hivyo kunogesha tukio la ghafla na kulifanya liwe la manufaa kwa wasikilizaji.

Baadhi ya wasikiliza wa kipindi cha Leo Tena kilichorusha mahojiano hayo, waliambia TPJ kwamba majibu ya Manasseh yaliwatoa matongotongo vilivyo juu ya nafasi ya PPRA katika kufanikisha maendeleo ya wananchi – hasa katika kusimamia mfumo wa National e-procurement System of Tanzania, au NeST, ili Serikali iweze kukabili ulaghai wa wazabuni wanaoitia hasara kwa kuweka kwenye zabuni zao bei za juu zaidi kuliko uhalisia.

Kwa mujibu wa wasikilizaji hao, maswali yalivyoulizwa kulimfanya Manasseh atoe majibu kwa ufasaha zaidi na maelezo yaliyokata kiu ya kujua uwezo wa NeST katika kuleta uwazi na usawa na inavyowezesha uzuiaji wa bei za juu kupindukia katika tenda na adhabu kwa wazabuni wanaoshindana kifisadi.

Manasseh apangua maswali ya Clouds FM kuhusu...



Manasseh alitumia fursa hiyo pia kuelezea jinsi NeST inavyofanikisha uwajibikaji na tija katika ununuzi wa umma, kwa staili iliyoweka wazi kwamba PPRA inayo majibu sahihi kwa maswali yote – ilimradi yaulizwe kwa staili yenye lengo la kupanua wigo wa uelewa.

Nukuu Kutoka Kwa Washiriki:

- ✓ “Hili ni tukio la kipekee. Hatukutarajia Meneja wa Kanda awe tayari kiasi hiki. Ameelezea NeST kwa namna ambayo hata sisi wananchi wa kawaida tumeelewa kwa urahisi.”— **Mshiriki wa maonyesho, Mtwara**
- ✓ “Majibu yake yametoa picha ya jinsi PPRA inavyolinda maslahi ya taifa dhidi ya watoa zabuni wasio waaminifu.”— **Mwandishi wa Clouds FM**

Mwigulu: Mifumo haina mbadala, lazima tutumie NeST...

Katika hatua nyingine, waziri aliielekeza PPRA kuhakikisha inafuatilia uzingatiaji wa sheria ili taasisi nunuzi zitenge kiasi cha asilimia 30 ya bajeti zake za ununuzi kwa ajili ya makundi maalum, yaani wanawake, wazee, vijana na watu wenye ulemavu.

“Sheria hii imeweka asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi kwa ajili ya makundi maalum; wekeni njia inayopimika ili hii fursa ipimike, “alisema na kusisitiza: “Tuwape nafasi.”

Aidha, alisisitiza umuhimu wa taasisi za umma kutumia ipasavyo fursa ya upendeleo inayotolewa na sheria ya ununuzi wa umma kuhusu bidhaa, watu na kampuni za ndani.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa PPRA, Dkt. Leonada Mwagike alisema pamoja na mambo mengine, katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Mamlaka hiyo imewajengea uwezo wadau kuhusu NeST na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 kwa jumla ya washiriki 8,904 kutoka taasisi nunuzi 2,020.



UNUNUZI WA UMMA SASA RAHISI NA WA UWAZI KUPITIA NeST!

- ✓ **Hakuna Mbadala wa Matumizi ya Mifumo!** – Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, amesisitiza kuwa taasisi za umma lazima zitumie Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (NeST) kwa uwazi na uwajibikaji zaidi.
- ✓ **Fursa kwa Makundi Maalum!** – Asilimia 30 ya bajeti za ununuzi zinapaswa kutengwa kwa wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu.
- ✓ **Hakuna Njia za Mkato!** – NeST imeondoa mianya ya udanganyifu, na sasa kila mtanzania anaweza kushiriki kwenye zabuni za serikali kwa haki na usawa.

📌 *“Changamoto tutazitatua, lakini lazima twende na mifumo na hatuna mbadala.” – Dkt. Mwigulu Nchemba*

NeST ni ufunguo wa maendeleo – Jisajili leo!

PPRA yawataka wataalam wa ununuzi na ugavi kuzingatia sheria, kutumia NeST

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Bw. Dennis Simba, amesisitiza umuhimu wa taaluma ya ununuzi na ugavi kama msingi wa utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati nchini, akiwataka wataalamu katika sekta hiyo kupalilia kiu ya kuongeza weledi na ubunifu.

Akizungumza katika ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Nne wa Chama cha Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi, APSP, uliofanyika kwenye kituo cha kimataifa cha mikutano kilichopo Arusha, AICC, Bw. Simba aliipongeza APSP kwa jitihada zake za kuboresha taaluma hiyo na kuisitiza kwamba uzembe katika sekta ya ununuzi wa umma una uhusiano hasi na utafutaji wa thamani ya fedha kwenye miradi ya maendeleo.



"Taaluma ya ununuzi na ugavi ni mhimili wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati nchini. Ukosefu wa weledi unaweza kusababisha miradi hiyo kutekelezwa chini ya kiwango, jambo linaloathiri maendeleo ya taifa," alisema Bw. Simba.

Aidha, Bw. Simba aliwataka wataalamu hao kubadili mtazamo wao na kutumia mifumo ya kisasa, kama NeST, akisema kuwa mfumo huo umewekwa ili kuhakikisha kunakuwapo uwazi na usawa katika ununuzi wa umma.

"Hakuna nafasi ya 'connection' [kujuana] katika ununuzi wa umma. NeST inahakikisha kila hatua inafanyika kwa uwazi na kwa mujibu wa sheria," aliongeza Bw. Simba huku akisisitiza kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wanaokiuka sheria.

PPRA yawataka wataalam wa ununuzi na ugavi...

Mwenyekiti wa APSP, Bw. Emmanuel Urembo, ameishukuru PPRA kwa kutambua nafasi ya chama hicho sambamba na kuona umuhimu wao katika sekta ya ununuzi wa umma.

Pia, Bw. Chaurembo ameahidi kutoa ushirikiano wa kujadili hoja za kitaaluma katika sekta hiyo nyeti nchini ili kuibua mambo yatakayosaidia jitihada za kuboresha ununuzi wa umma.

Katika hatua nyingine, Bw. Simba aliahidi kuwa PPRA itachangia Shilingi milioni 25 kusaidia ununuzi wa kiwanja cha APSP jijini Dodoma, huku akiwasihi wanachama wa chama hicho kushirikiana kufanikisha ndoto hiyo.

Mkutano huo, ulijadili mada mbalimbali zinazohusiana na kaulimbiu “Taaluma, Thamani na Kujenga Uwezo” na ulihudhuriwa na zaidi ya wataalamu 150 kutoka kada ya ununuzi na ugavi nchini.



UNUNUZI WA UMMA WALETA MAPINDUZI – WATAALAMU WAASWA KUZINGATIA NeST!



Ununuzi wa Umma ni Muhimu kwa Maendeleo! – Mkurugenzi Mkuu wa PPRA, Bw. Dennis Simba, ameweka wazi kuwa taaluma ya ununuzi na ugavi ni nguzo ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati nchini.



NeST Ni Lazima! – Mfumo wa ununuzi wa umma NeST umeimarisha uwazi na uwajibikaji, huku ukiondoa nafasi ya ‘connection’ zisizo rasmi katika ununuzi wa umma.



Wataalamu Kuhamasika! – Zaidi ya wataalamu 150 kutoka kada ya ununuzi na ugavi walihudhuria mkutano uliobeba kauli mbiu ya “Taaluma, Thamani na Kujenga Uwezo”, ambapo PPRA iliahidi kushirikiana na APSP kuboresha mazingira ya ununuzi.

“Hakuna mbadala wa matumizi ya mifumo, lazima twende na NeST ili kuweka uwazi na kuhakikisha haki inatendeka.” – Bw. Simba

NeST – Mfumo Salama, Wazi na Wa Haki kwa Wote!

PPRA yawanoa wenye ulemavu matumizi ya NeST kuomba tenda

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imetoa mafunzo kwa watu wenye ulemavu ili kuwajengea uwezo wa kujisajili na kuomba tenda kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa manunuzi ya umma, yaani NeST.

Mafunzo hayo, yaliyofunguliwa jijini Dodoma Novemba 15, 2024 na Mkurugenzi wa Idara ya Walemavu katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Rashid Maftah, yalilenga kuwawezesha waliomo katika kundi kunufaika na fursa zilizomo kwenye zabuni za umma.

Katika hotuba yake, Bw. Maftah aliwaasa washiriki kuyapa mafunzo hayo uzito stahiki “kwani yatawawezesha kupata uelewa juu ya fursa zilizoinishwa kwenye sheria ya ununuzi wa umma kuhusu zabuni za umma.”

“Pia, mtapata uelewa] juu ya mfumo uitwao NeST ambao ndio njia pekee inayotumika kuomba zabuni za serikali kwa mujibu wa sheria,” alisema na kasisitiza: “Hakuna kabisa utaratibu mwingine wa kuomba zabuni za serikali nje ya NeST.”

“Mafunzo haya yatawawezesha kupata fursa ya kuomba zabuni za serikali, kujipatia ajira na kuajiri wengine na kuondokana na umaskini,” alisema Maftah.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PPRA Salmin Malole, alizungumzia mageuzi makubwa yaliyofanywa na Serikali kwenye sekta ya ununuzi wa umma, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, ikiwemo NeST na marekebisho yaliyozaa sheria ya ununuzi wa umma ya Mwaka 2023 na kanuni zake za Mwaka 2024.

“Yote haya yameongeza wigo wa fursa kwa wataanzania na kurahisisha upatikanaji wake kwa uwazi na usawa,” Bw. Malole alisema na kubainisha kuwa mafunzo hayo ni mwendelezo wa programu ya PPRA ya kuwajengea uwezo wadau wa ununuzi wa umma mwaka wa fedha 2024/2025.

“[Pamoja na ukweli kwamba] Serikali imetoa fursa ya upendeleo kwa wataanzania wote, kuna ule wa makundi maalum ambayo ni vijana, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu,” alisema Malole na kuongeza kuwa makundi haya yametengewa asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi wa umma, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya Serikali kwa wananchi.

“Wananchi wanaweza kujiunga kwenye vikundi vyenye watu watano hadi 20 na wakapata fursa hizi,” alisema.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali, linalojihusisha na masuala ya watu wenye ulemavu, Michael Salali, watu hawa bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo sheria ya watu wenye ulemavu ya Mwaka 2009.

NeST yaibuka mfumo bora zaidi wa ununuzi wa umma Afrika

Mfumo wa usimamizi wa ununuzi wa umma kielektroniki, NeST, umeshinda tuzo ya “Mfumo Bora wa Ununuzi wa Umma Barani Afrika,” kati ya tuzo za African Association for Public Administration and Management (AAPAM), zilizokuwa zikishindaniwa chini ya uangalizi wa Umoja wa Afrika (AU), jijini Kampala, Uganda.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Kampala, baada ya kupokea tuzo hiyo mbele ya mamia ya washiriki wa Mkutano wa AAPAM, Novemba 28, 2024, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), inayosimamia NeST, Bw. Dennis Simba, alisema kuwa tuzo hii ni heshima kubwa kwa Tanzania, kwani ununuzi wa umma ni moja ya maeneo yanayotumia asilimia kubwa ya fedha za umma barani Afrika.

"Tuzo hii imetuletea heshima kubwa, kwani tulifika katika tano bora kati ya washiriki 69 na ni sisi pekee ambao tumeingiza mfumo wa ununuzi wa umma na leo umetambulika na kupewa tuzo hii... ni mafanikio makubwa kwa Tanzania na kwa mfumo wetu," alisema Bw. Simba na kuelekeza pongezi za kipekee kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyewezesha kuanzishwa kwa sheria ya ununuzi wa umma ya Mwaka 2023, na kuundwa kwa NeST."



NeST yaibuka mfumo bora zaidi wa ununuzi wa...

Bw. Simba alisema kwa kuwa mfumo huu umejengwa na wataalam wa Tanzania pekee, PPRA iko tayari kushirikiana na nchi nyingine kuhakikisha kuwa teknolojia hii inawafikia na kusaidia katika mageuzi ya sekta ya ununuzi wa umma barani Afrika.

Ameishukuru Wizara ya Fedha kwa kuwezesha ujenzi wa mfumo huu na ufuatiliaji wake wa hatua zote kuhakikisha maono ya Rais Samia yanatekelezwa. Aidha, alisema kuwa ujenzi wa mfumo huu umewezekena kupitia ushirikiano kati ya PPRA na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) waliotoa wataalam na miongozo.

Kwa upande mwingine, mfumo wa kutoa huduma ya afya kwa jamii nchini Kenya umeshinda tuzo ya jumla, huku Uganda ikikabidhiwa Tuzo Maalum kwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa AAPAM.



Sababu Gani NeST Ni Ya Kipekee?

- ✓ **Imejengwa na Wataalamu wa Kitanzania** – Teknolojia ya ndani kwa asilimia 100
- ✓ **Inaongeza Uwajibikaji na Uwazi** – Manunuzi yanafuatiliwa kwa uwazi kila hatua
- ✓ **Imetambuliwa Kimataifa** – Imechaguliwa kutoka miongoni mwa mifumo ya nchi 69
- ✓ **Tanzania Tayari Kwa Ushirikiano** – Inakaribisha mataifa mengine kujifunza mfumo huu

TAARIFA KWA TARAKIMU



14

Thamani ya mikataba yote katika triloni za shilingi, ikihusisha zabuni zilizotolewa kupitia NeST, hadi februari 2025.

JE, WAJUA?

Sasa zabuni za umma zinatolewa kupitia NeST hadi kijiji katika serikali za mitaa.



Mwigulu: Mifumo haina mbadala, lazima tutumie NeST



Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba amezitaka taasisi za umma nchini kuhakikisha zinatumia mfumo wa ununuzi wa umma kielektroniki, NeST, kwa kuwa hakuna mbadala wa matumizi ya mifumo.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam alipokuwa akipokea Taarifa ya Tathmini ya Utendaji Kazi ya Mamlaka ya Udhubiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

Dkt. Nchemba alisema kuwa mfumo NeST, ulioanza kutumika Julai 2023, umeongeza uwazi na uwajibikaji na umesaidia kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani wa taasisi nunuzi, na hivyo kuendana na maelekezo ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyeitaka Wizara ya Fedha kudhibiti matumizi ya fedha za serikali - hasa kwenye utekelezaji wa miradi.

“Natambua kuwa kuna changamoto zinazoweza kujitokeza, lakini hatuna mbadala, lazima twende kwenye matumizi ya mifumo,” alisema na kuongeza kuwa katika maeneo fulani mifumo huwa inatajwa kuwa na changamoto kwa lengo la kukataa na kuendelea na njia wanazozitaka wao kwa maslahi yao binafsi.

“Ili watu waukatae mfumo, watauhusisha na kila tatizo linalowakabili kwa manufaa yao tu... changamoto za msingi tutazitatua, lakini lazima twende na mifumo na hatuna mbadala na lazima isomane,” alisema Dkt. Nchemba.

Aliitaka PPRA kuendelea kutoa mafunzo kwa wadau wa ununuzi ili kuhakikisha kuwa ukosefu wa uelewa wa matumizi ya NeST hauwi kikwazo cha kuwaletea maendeleo watanzania. Pia, aliitaka Mamlaka hiyo kuwachukulia hatua za kisheria wale ambao watakataa kutumia mfumo huo kwa makusudi.

DC Mtwara awaasa wananchi kuchangamkia zabuni za Serikali

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Abdallah Mwaipaya, amewataka wananchi kuchangamkia fursa zinazopatikana katika zabuni za umma ili wanufaike na ununuzi unaochukua zaidi ya asilimia 70 za bajeti ya Serikali, imefahamika,

Bw. Mwaipaya aliyasema hayo wakati akifungua rasmi Ofisi za PPRA Kanda ya Kusini, zilizopo katika Jengo la PSSSF – Sokoine, Mtwara Mjini, Februari 28, 2025.

Aidha, mkuu huyo wa wilaya alisema litakuwa jambo jema kama wananchi wengi watafanya uamuzi wa kuunda kampuni au vikundi vya watu angalau watano hadi ishirini, ili waweze kunufaika na fursa katika miradi kwani Serikali inatekeleza miradi mingi mkoani Mtwara.

Hata hivyo, Bw. Mwaipaya alitumia fursa hiyo kuwambusha wananchi kuhusu hatua inayofuata, yaani kujisajili kwenye NeST, mfumo wa taifa ambao kwa sasa ndio njia pekee ya kupata fursa ya zabuni za umma na kwamba endapo watakumbana na changamoto yoyote, waende kwenye Ofisi za PPRA kupata msaada na ufafanuzi, kwa vile sasa huduma zimesogezwa karibu.

Vilevile, aliwataka watumishi wa umma kuzingatia matakwa ya sheria kwa kutumia NeST kufanya ununuzi wa umma na kwamba wajiepusha na visingizio dhidi ya matumizi ya mfumo huo unaoongeza ufanisi, uwajibikaji, na uwazi na kuzuia upotevu wa fedha za umma kwenye michakato ya ununuzi.

“Mheshimiwa Rais aliagiza mifumo isomane...tunaona NeST, mfumo ambao mwaka jana tu ulipata tuzo ya kuwa Mfumo Bora wa Ununuzi wa Umma kwa Ubunifu - Afrika, umeunganishwa na mifumo 20 hadi sasa. Niipongeze PPRA kwa jitihada hizi, na sisi tuendeleo kuutumia kupata fursa na kupata thamani halisi ya fedha hususan kwenye miradi ya kuwaletea maendeleo wananchi wetu,” amesema Mwaipaya.

Tukio la uzinduzi wa ofisi za PPRA Kanda ya Kusini liliambatana na semina kwa waandishi wa habari takribani 50 wa Mkoa wa Mtwara, iliyofunguliwa na mkuu huyo wa wilaya.

Manasseh: NeST ndiyo ‘koneksheni’ pekee katika kushinda tenda za Serikali

Meneja wa PPRA Kanda ya Kusini, Bw. Finias Manasseh, amewataka wananchi kuchangamkia tenda za Serikali bila kuhofia kwamba tenda zao zitachezewa na watumishi wa umma wasio waaminifu kwani NeST imekata njia zote za rushwa na udanganyifu katika ununuzi wa umma.

Manasseh aliyasema hayo Februari 28, 2025 katika Jengo la PSSSF – Sokoine, Mtwara Mjini, kwenye semina mahsusi iliyoandaliwa na kuendeshwa na PPRA kwa ajili ya kuwaongezea waandishi wa habari uelewa kuhusu ununuzi wa umma ili katika ili shughuli yao ya kuufikishia umma ujumbe sahihi iwe rahisi zaidi.

Aliongeza kuwa PPRA imejipanga kutoa huduma itakayofanikisha ununuzi wa umma kwa Watanzania katika mikoa yote, ili kuhakikisha kuwa lengo la Serikali la kuwainua wananchi kiuchumi na kuwaletea maendeleo endelevu linatimia.

Manasseh alisisitiza kuhusu nafasi ya NeST katika kufanikisha malengo ya kitaifa kwa kusema: “Katika ununuzi wa umma hakuna kujuana maana ‘connection’ pekee ya tenda za Serikali ni NeST,” na aliwashauri waandishi kufikisha ujumbe kwa wananchi kwamba wanaweza kushiriki michakato ya ununuzi wa umma popote walipo, kupitia mfumo huo kwa uwazi, usawa na bila mambo ya kujuana na mtu yeyote.

Aliishukuru Serikali, kwa niaba ya Menejimenti ya PPRA, kwa kuwezesha ufunguzi wa Ofisi za Kanda pamoja na kwa kuhakikisha Sheria ya Ununuzi wa Umma inatoa fursa za kipekee kwa Watanzania kuanzia ngazi ya chini kabisa ya vijiji na mitaa hadi ya Taifa.

NeST Kama Daraja la Maendeleo

KWA MUJIBU WA BW. MANASSEH, MFUMO WA NEST SI TU JUKWAA LA KIUFUNDI, BALI NI NGUZO YA KIUCHUMI, INAYOWEZESHA:

- ✓ Mtanzania wa kawaida kushiriki kikamilifu kwenye miradi ya maendeleo
- ✓ Kuondoa vikwazo vya mazoea ya kujuana, rushwa na ubaguzi
- ✓ Kuinua uwazi na ushindani kwa maslahi ya taifa

TANZANIA PROCUREMENT JOURNAL

ISSN: 1821– 6021 – March, 2025



 0736494948

 www.ppra.go.tz

 dg@ppra.go.tz